

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



"Nyamagana" Posta Road,  
S.L.P. 2599,

33101 MWANZA,  
Barua Pepe: rbcmwanza@pccb.go.tz.

**TANZANIA.**

[www.pccb.go.tz](http://www.pccb.go.tz)

---

**MWANZA – FEBRUARI 25, 2021**

**TAARIFA KWA UMMA**

**AFISA UVUVI ILEMELA AFIKISHWA MAHAKAMANI KWA KOSA  
LA RUSHWA**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wilaya ya Ilemela Mkoani Mwanza, imemfikisha Mahakamani Afisa Uvuvi Bw. CHARLES EUSEDIUS ARAJIGA (37) kwa kosa la kuomba na kupokea Rushwa kinyume na Kif cha 15 (1) (a) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya mwaka 2007.

Afisa uvuvi huyo Bw. CHARLES EUSEDIUS ARAJIGA (37) amekamatwa na Maafisa wa TAKUKURU tarehe 20 Februari 2021 kwa kosa la kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 80,000/= kutoka kwa wafanyabiashara wadogo wa samaki wa Soko la Sabasaba lililopo katika Manispaa ya Ilemela jijini Mwanza.

Bwana ARAJIGA amekuwa kero ya muda mrefu katika soko hilo, kwani alijiwekea utaratibu wa kila wiki kuwa anapokea shilingi laki moja (100,000/=) kutoka kwa wafanyabiashara hao wadogo wa samaki kwa madai kwamba asiwe anawasumbua katika shughuli zao.

Chanzo cha siri cha taarifa zetu kinasema pindi wafanyabiashara hao wanaposhindwa kumpatia Sh. 100,000/= kwa wiki, Afisa Uvuvi huyo anachukua samaki zote bila sababu za msingi na ili wazikomboe sharti walipe Sh. 700,000/=. Aidha, wanaposhindwa kulipa hiyo fedha kiasi cha sh 700,000/= Afisa uvuvi huyo anauza samaki zote na kuwaacha wafanyabiashara hao wakiwa hawana mitaji.

Uchunguzi wa TAKUKURU mkoa wa Mwanza ulibaini kuwa, Wafanyabiashara hao baada ya ya kunyanyasika kwa muda mrefu ndipo walipomwambia Afisa Uvuvi huyo Bwana ARAJIGA kuwa kwa sasa hali ni ngumu hawataweza kutoa shilingi laki moja kila wiki.

Uchunguzi huu ulibaini pia kuwa ilifikia hatua wafanyabiashara wamechoshwa na tabia ya Afisa huyo ndipo walipoamua kufunguka na kutoa taarifa TAKUKURU Wilaya ya Ilemela ambapo mtego ukaandaliwa na Bw. ARAJIGA akakamatwa kwa kosa la kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 80,000/= kinyume na Kif cha 15 (1) (a) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007.

Uchunguzi wa tuhuma hii umekamilika na leo tarehe 25 Februari, 2021 Afisa Uvuvi huyo Bw. CHARLES EUSEDIUS ARAJIGA (37) amefikishwa

katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Ilemela na kufunguliwa shauri la rushwa namba 01/2021 kujibu tuhuma zinazomkabili.

Akisomewa mashtaka yake na Mwendesha mashtaka wa TAKUKURU Moses Malewo mbele ya Hakimu Mkazi Mheshimiwa Kubaja Fortunatus, mtuhumiwa amekana mashtaka yanayomkabili.

Aidha, Mtuhumiwa yuko nje kwa dhamana kwa masharti ya kuwa na wadhamini wawili na kila mmoja awe na mali yenye thamani ya Sh. 2,000,000/=. Kesi hiyo itaendelea kusikilizwa tena tarehe 09/03/2021.

### **WITO:**

TAKUKURU Mkoa wa Mwanza inaendelea kuwahimiza watumishi na wananchi wote kwa ujumla kuwa waaminifu kwenye utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku, lakini pia washiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kutoa taarifa za vitendo vya rushwa ili wahusika wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria.

**“Kwa taarifa za vitendo vya rushwa fika ofisi ya TAKUKURU iliyo karibu nawe, tumia TAKUKURU APP, piga simu ya dharura namba 113 au tuma ujumbe mfupi wa maneno kwenda namba 113 au Piga \*113# fuata maelekezo” Huduma hii ni ya BURE**

### **IMETOLEWA NA:**

.....

**FRANK MKILANYA – 0738 150 162**

**MKUU WA TAKUKURU (M) MWANZA**